JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Simu/Fax: +255 232935205

Barua pepe: dakawatc@moe.go.tz

Chuo cha Ualimu Dakawa,

S. L. P. 944,

MOROGORO.

Tarehe: 13/05/2022

Kumb. Na. ***DKWTC/JSTR/VOL.1/***

Ndugu**……**

S.L.P. **……**

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI (ENGLISH MEDIUM) NA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU SEKONDARI KWA MWAKA 2022/2023.

1.0 UTANGULIZI

Napenda kukupongeza na kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya; Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi **(English Medium)**/Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari katika Chuo cha Ualimu Dakawa.

Ukiwa Chuoni utapewa muda wa kufanya Mazoezi ya kufundisha kulingana na kalenda ya chuo. Tunasisitiza kuwa uthamini uchaguzi huu kwa kusoma kwa bidii na kufuata taratibu na kanuni za chuo.

2.0 MAHALI CHUO KILIPO

Chuo Cha Ualimu Dakawa kipo **Mkoa wa Morogoro,** Wilaya ya Kilosa, Umbali wa kilometa **60** kutoka Morogoro Mjini, Barabara Kuu iendayo **Dodoma.** Ukifika **Msamvu, Morogoro**, Stendi Kuu ya mabasi, uliza stendi ya magari madogo (Daladala au Noah) yaendayo **Dumila.** Shuka njia panda ya **VETA Dakawa.** Pia, ukitokea Dodoma; Shuka njia panda ya **VETA Dakawa**. Kisha, chukua usafiri wa pikipiki, wakulete chuo cha Ualimu Dakawa, umbali wa kilometa nne (**4)** tu kutoka barabara kuu. Nauli ya pikipiki si zaidi ya **Tshs. 3,000/=**

N.B Unashauriwa kufika mapema kabla ya saa 11:00 jioni kwa ajili ya usalama.

3.0 KUFUNGUA CHUO

Unatakiwa kufika chuoni tarehe **13/06/2022** na mwisho wa kufika chuoni ni tarehe **31/06/2022** bila kukosa. Utakapofika chuoni nenda **Ofisi ya Usajili** ambapo utapata maelekezo na taratibu zote za chuo na kusajiliwa.

Kukamilisha Usajili unatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo:

3.1 Barua ya kuitwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu (Joining Instruction).

3.2 **Vyeti halisi vya kuhitimu** (Leaving Certificates) Kidato cha **nne** au Kidato cha sita, ama vyote.

3.3 Vyeti halisi vya kufuzu (Academic Certificates) Kidato cha nne au Kidato cha sita ama vyote Au Result Slip kwa wale waliomaliza Kidato cha nne mwaka 2021 na Kidato cha Sita mwaka 2022.

3.4 Cheti halisi cha kuzaliwa (Original birth certificate).

3.5 Walioajiriwa walete barua za ruhusa ya kuhudhuria mafunzo kutoka kwa Waajiri wao.

3.6 Uje pia na vivuli **(photocopies)** vya vyeti vyako vyote.

3.7 Fomu ya kupimwa Afya na Daktari wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya (fomu imeambatanishwa pamoja na barua hii).

3.8 Picha mbili za rangi (passport size).

3.9 Uje na Kitambulisho cha BIMA YA AFYA ikiwa unacho.

NB: Kumbuka hutapokelewa chuoni iwapo hautawasilisha nyaraka tajwa hapo juu.

4.0 ADA

Ada ya Mafunzo ya Ualimu ni **Tsh. 450,000/= kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa yote kwa mkupuo** au kwa awamu mbili Tsh. **225,000/=** kwa kila muhula. Ada italipwa kwa mtandao (GEPG) baada ya kutengenezewa namba ya malipo (**Control number)** na Mhasibu wa Chuo mara ufikapo chuoni.

4.1 Utapaswa kulipa Ada ya Mtihani wa Ualimu wa mwisho kiasi cha shilingi 50,000/= kwenda Baraza la Mitihani.

5.0 FEDHA YA MICHANGO

Utatakiwa kulipa Fedha ya Michango kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo chini;

S/N	MCHANGO	KIASI	MAONI
1	Serikali ya wanachuo	5,000/=	Kwa Mwaka
2	Huduma ya kwanza	10,000/=	Kwa Mwaka
3	Usafi na mazingira	20,000/=	Kwa Mwaka
4	Kukodisha godoro	10,000/=	Kwa Mwaka
5	Usajili na Kitambulisho	20,000/=	Kwa Mwaka
6	Michezo	30,000/=	Kwa Mwaka
7	Ulinzi	30,000/=	Kwa Mwaka
8	Ukarabati na matengenezo	25,000/=	Kwa Mwaka
9	Bima ya Afya ya Taifa	50,400/=	Kwa wasio na Bima ya Afya
10	Kukodi vazi la mahafali (Joho)	15,000/=	Kwa mwaka wa pili tu

	JUMLA	**215,400/=**	

N.B Hakikisha malipo ya fedha ya michango yote yaingizwe kwenye **Akaunti ya Chuo cha Ualimu Dakawa, Namba 01J1048471300; Jina la Akaunti ni; DAKAWA T.C - SELF RELIANCE A/C - CRDB. Mandela Branch Morogoro. Lipa kwenye tawi lolote la CRDB lilipo karibu nawe kisha uje na BANK PAY SLIP.** Usije na fedha taslimu ya Michango haitapokelewa.

6.0 SARE YA CHUO

6.1 Vazi rasmi la Chuo ni Uniform pair mbili. Suruali mbili za rangi nyeusi zenye mashono ya heshima ***(isiwe modal),*** mifuko mitatu, rinda mbili na turn up. Mkanda wa ngozi mweusi na soksi nyeusi (Wavulana). Sketi mbili nyeusi ndefu zenye mshono wa mapande sita (6) (kitambaa cha suti) zisizo na mpasuo, zinazovuka magoti nchi tatu na soksi nyeupe (Wasichana).

6.2 Koti jeusi la suti rangi ya suruali au sketi na tai ndefu (Wavulana) na Wasichana tai nyeusi fupi (siyo butterfly).

6.3 Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya light blue yanapatikana chuoni kwa **sh. 30,000/=** kwa yote mawili.

6.4 T-Shirt yenye rangi ya bluu bahari inapatikana chuoni kwa shilingi **15,000/=**

6.5 Viatu vya ngozi vya kufunika na soksi nyeusi kwa wavulana na soksi nyeupe kwa wasichana.

6.6 Wanachuo wa kike watakaopenda kuvaa Hijab watumie rangi ya Light Blue (*Ifanane na shati*) urefu usawa wa kifua.

6.7 Nguo za michezo, Tracksuit ya bluu pair 1, bukta ya bluu 1 na fulana ya bluu (**Bluu ya kuiva ‘’deep blue’’**), raba jozi 1, pamoja na nguo nyingine za michezo kama sketi (wasichana) n.k

5.0 VIFAA/MAHITAJI MENGINE MUHIMU

5.1 Blanketi 1, shuka mbili za light blue zisizofumwa, foronya 2 za light blue, mto 1, pamoja na chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu.

5.2 Vyombo vya chakula; sahani1, bakuli 1, kijiko 1, Kikombe 1 **(visiwe vya plastic) na** galoni ya plastiki ya lita 5 ya kuhifadhia maji ya kunywa.

5.3 Ndoo ya kuogea. (*Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo)*

5.4 Tochi yenye betri kwa ajili ya tahadhari ya kukosekana kwa umeme.

5.5 Pazia light blue urefu wa ft. 9 kwa ft. 3.5 kwa ajili ya chumba chako.

5.6 Daftari kubwa zisizopungua 10 kwa muhula (kaunta book Quare 2) *(hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo.*

5.7 Vitabu mbalimbali na Mihtasari ya michepuo ya masomo yako uliyochaguliwa.

5.8 Rimu moja ya karatasi nyeupe aina ya NO 1/mondi nyeupe (A4 photocopy paper) kwa ajili ya shughuli za kitaaluma. Hii hutolewa kila mwaka *(Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo).*

5.9 Kwa mwanachuo atakayesoma somo la Hisabati aje na ‘’scientific calculator’’ na ‘’mathematical table’’.

MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA WANACHUO

a. Unashauriwa kuja na sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako.

b. Unashauriwa kuja na rimu moja kwa ajili ya matumizi yako binafsi.

c. Unashauriwa kuja na fedha taslimu kwa ajili ya matumizi binafsi.

d. Unashauriwa kuja na mavazi mengine mbali ya sare ila yawe ya mashono ya *Heshima na yanayoakisi Taaluma ya Ualimu.* (Mavazi hayo yatakaguliwa ofisi ya Usajili).

6. MWISHO:

Katika kipindi chote cha mafunzo mwanachuo atatakiwa kutii sheria za Nchi, za Chuo na Kanuni za mwenendo bora wa mwanachuo. Ufikapo chuoni utakabidhiwa nakala ya sheria, kanuni za taratibu za Chuo. Pia utatakiwa kukiri au kukubali nafasi hiyo ya mafunzo kwa kujaza fomu.

“***Ualimu bora huanzia chuoni; Tunakutegemea kuwa Mwalimu bora tangu mwanzo wa mafunzo yako”.***

KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU DAKAWA

PRINCIPAL
DAKAWA TEACHER'S COLLEGE
P. O. BOX 944, MOROGORO

DOROTHY I. MHAIKI

MKUU WA CHUO

Kwa Mawasiliano:

0767259510-Mkuu wa Chuo

0756 484454-M/Mkuu wa Chuo

0657104040-Mhasibu

0764019518-Msajili

Nakala: Mkurugenzi Elimu ya Ualimu,
Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia,
S. L. P .10
40479 DODOMA

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To:
The Medical Officer
……..
……...
……..

Mr/Mrs/Miss ……
(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course.
The examination should include the following categories (i – ii) each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Primary/category iv will also render a girl candidate ineligible for the course:-

i. (a) Eye-sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech
(e) Venereal disease (f) Leprosy (g) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious diseases
iv. Pregnancy

MEDICAL CERTIFICATE

PART B: (To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training course.

i. (a) Eye-sight…… (b) Hearing…… (c) Limbs ……
(d) Speech……. (e) Venereal diseases…….
(f) Leprosy …… (g) Epilepsy……
ii. Neuroses ……
iii. Serious diseases…….
iv. Pregnancy

Date …….. **Signature** ……

Station …… **Designation** …….